
THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

Supplement No. 44

29th October, 2021

SUBSIDIARY LEGISLATION

to the Gazette of the United Republic of Tanzania No.44. Vol.101 dated 29th October, 2021
Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 774 la tarehe 29/10/2021

SHERIA YA KUDHIBITI SILAHA NA RISASI,

(SURA YA 223)

NOTISI

(Imeandaliwa chini ya kifungu cha 64)

Jina **1.** Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Msamaha Kwa Watu Wanaosalimisha Silaha, 2021.

Msamaha wa kutoshtakiwa **2.**-(1) Mtu yeyote ambaye anamiliki silaha kinyume na Sheria ikiwa atasalimisha silaha hiyo katika kipindi cha kuanzia tarehe 1 Novemba, 2021 mpaka tarehe 30 Novemba, 2021 atapewa msamaha na hatashtakiwa kutokana na uamuzi wake wa kusalimisha silaha hiyo.

(2) Maeneo ya kuwasilisha silaha kwa mujibu wa aya hii yatakuwa ni-

- (a) Vituo vya Jeshi la Polisi
- (b) Ofisi za Serikai za Mitaa; na
- (c) Ofisi za Watendaji wa Kata.

Muda wa kusalimisha silaha **3.** Muda wa kusalimisha silaha utakuwa ni kuanzia saa mbili asubuhi mpaka saa kumi jioni kila siku kwa kipindi kilichoainishwa katika aya ya 2.

Dodoma
25 Oktoba, 2021

GEORGE BONIFACE SIMBACHAWENE
Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi